3. Baada ya kutengeneza akaunti mwombaji atatumiwa jina la kutumia kwenye akaunti yake pamoja na link ili "ku-activate" akaunti na kisha kuingia kwenye akaunti yake kwa ajili ya kupata huduma zinazotolewa.
4. Mteja atakapoingia kwenye akaunti yake atachagua sehemu ya "huduma mtandao" (new e-service).
5. Ndani ya huduma mtandao kuna huduma zote zitolewazo na BRELA ambazo ni Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Leseni za Viwanda na huduma za taarifa, mteja atachagua huduma anayohitaji Hataza.
6. Mteja anapochagua Hataza mfumo utamuwezesha kuingiza taarifa za usajili mpya au maombi mengineyo yanayohusiana na Hataza.
7. Mtumiaji wa mfumo atachagua huduma ya usajili wa Hataza.
8. Mwombaji atachagua maombi mapya ya hataza.
9. Ataingiza taarifa za uwakilishi (Representation Statement), hapa atasema mwombaji anaomba kama nani, mmiliki au mwakilishi.
10. Mwombaji ataingiza maelezo ya kitaalam (Technical description)
11. Atachagua aina ya maombi kama ni ya "PCT" (hataza ya kimataifa kupitia Shirika la Miliki Ubunifu la Dunia) au aina nyingine (other) ambapo atachagua aina ya hataza
12. Atajaza kichwa cha habari cha uvumbuzi
13. Ataweka maelezo ya utangulizi ya uvumbuzi
14. Ataonyesha rejea ya namba ya mwisho ya ukurasa wa madai ya uvumbuzi (claims)
15. Mwombaji ataweka rejea ya namba ya ukurasa wa mwisho wa maelezo ya hitimisho ya uvumbuzi (description)
16. Ataweka maelezo ya dhahania ya uvumbuzi (Abstract)
17. Atajaza taarifa za madai ya uvumbuzi (claims)
18. Mwombaji atajaza taarifa za mmiliki wa Hataza
19. Atajaza taarifa za mwakilishi (Agent) kama maombi yanawasilishwa na mwakilishi.
20. Mwombaji atajaza taarifa za Mvumbuzi (inventor)
21. Mwombaji atajaza taarifa za maombi ya awali aliyowasilisha nchi nyingine ikiwa atataka tarehe itambulike hapa nchini kama ndio tarehe ya maombi (isizidi miezi 12 toka tarehe maombi yanawasilishwa katika nchi nyingine.
22. Ataonyesha kama hataza inahusiana na hataza ambayo ilishawasilishwa kabla (Divisions)
23. Baada yakuingiza taarifa zote atabonyeza kitufe cha endelea "proceed"
24. Mfumo utatengeneza fomu ambayo itakuwa na taarifa zote alizoingiza mteja "consolidated form" mteja atatakiwa kuidownload fomu, kuprint na kuweka sahihi zao na endapo mmiliki ni kampuni atatakiwa kugonga muhuri wake.
25. Mfumo utampeleka kwenye dirisha la kuambatanisha viambatanishi ambavyo ni ; fomu (consolidated form) kwenye muundo wa "PDF", atatakiwa kuambatanisha nyaraka/taarifa ya hataza (patent document), michoro wa hataza husika (kama ipo) ikiwa kwenye muundo wa "JPEG", kama kuna na "priority claim" atatakiwa kuambatanisha "priority documents", kama muombaji atakuwa ni muwakilishi atatakiwa kuambatanisha fomu Na. 1 ya uwakilishi.
26. Baada ya hapo atabonyeza kitufe cha endelea na mfumo utampeleka kwenye malipo ambapo atachagua njia ya malipo atakayotumia (simu au benki)
27. Mwombaji atachagua sehemu ya kukubali vigezo na masharti
28. Baada ya malipo maombi yanatumwa BRELA na mteja anaweza kuprint risiti yake kwa kubonyeza kitufe cha "download receipt"
29. BRELA watayafanyia kazi maombi
30. Baada yakukamilisha mteja anapokea ujumbe kwenye barua pepe na namba ya simu aliyoweka kwenye mfumo, ujumbe utamtaarifu matokeo ya ombi ambayo ayaona sehemu ya "maombi" (applications) atafungua ombi husika na ataweza kuona matokeo hayo sehemu ya "print-outs"
31. Kama ombi litakuwa na mapungufu atapokea ujumbe kwa barua pepe kumtaarifu kuhusu mapungufu ambapo kwenye ombi lake atapata maelekezo ya vitu vya kurekebisha kwa kufungua sehemu ya "my list" na kufungua ombi husika ili arekebishe. Akishafanyia marekebisho atatuma tena BRELA kwa ajili yakufanyiwa kazi.

HUDUMA KWA WATEJA:
0735 331 001, 0735 000003, 0735 331 004

BRELA

WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# HATUA ZA USAJILI WA ALAMA ZA BIASHARA NA HUDUMA NA HATUA ZA USAJILI WA HATAZA KWA NJIA YA MTANDAO

P. O. Box 9393, Dar es Salaam - Tanzania
Tel: +255 22 218 0139, 218 1344,
218 0113, 2180141, Fax: +255 22 218 0371
Email: usajili@brela.go.tz, ceo@brela.go.tz,
Web: www.brela.go.tz

## Hatua za Usajili wa Alama za Biashara na Huduma

1. Mtumiaji ataingia kwenye tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na kupata link ya usajili kwa njia ya mtandao

2. Mwombaji akishaingia kwenye kurasa ya usajili kwa njia ya mtandao (https://ors.brels.go.tz/ors) analazimika kufungua akaunti ili aweze kutumia huduma za BRELA zitolewazo kwa njia ya mtandao. Ili kutengeneza akaunti kwa mtanzania analazimika kuwa na namba ya utambulisho wa utaifa na kwa wasio raia watanzania namba ya pasi ya kusafiria pamoja na taarifa za barua pepe, namba ya simu ya mkononi na kutengeneza nywila (password).

3. Baada ya kutengeneza akaunti mwombaji atatumiwa jina la kutumia kwenye akaunti yake pamoja na link ili "ku-activate" akaunti na kisha kuingia kwenye akaunti yake kwa ajili ya kupata huduma zinazotolewa.

4. Mwombaji atakapoingia kwenye akaunti yake atachagua sehemu ya "huduma mtandao" (new e-service).

5. Ndani ya huduma mtandao kuna huduma zitolewazo na BRELA ambazo ni Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Leseni za Viwanda na huduma za taarifa, mteja atachagua Alama za Biashara na Huduma.

6. Mwombaji anapochagua Alama za Biashara na Huduma mfumo utamuwezesha kuingiza taarifa za usajili mpya au maombi mengineyo ya Alama.

7. Mwombaji atachagua huduma ya usajili wa Alama za Biashara na Huduma

8. Ataingiza taarifa zake za usajili kama ifuatavyo;

- Taarifa za muombaji zitaonekana na atatakiwa kuandika yeye anawasilisha ombi kama nani "representation statement"
- Atachagua ni kitu gani anataka kukilinda kama ni ulinzi wa bidhaa au huduma.
- Ataingiza taarifa za mmiliki/wamiliki ambazo ni; aina ya mtu natural or legal person, kama ni "natural person" atachagua urai endapo ni mtanzania atapaswa kuingiza Namba ya utaifa (NIDA No.) na mfumo utavuta taarifa ambazo ni pamoja na jina kamili la mmiliki wa namba hiyo ya utaifa kama ni "other" ambae ni kampuni, business name, other corporate body" atatakiwa kuingiza namba ya usajili wa Kampuni/ jina la biashara utabonyeza kitufe cha "search" Jina la kampuni/jina la biashara litajitokeza.
- Atatakiwa kujaza taarifa za anuani ya mmiliki/wamiliki.
- Kama mmiliki atachagua kutumia muakilishi "representative" atatakiwa kujaza taarifa zake
- Kama muombaji alishawahi kuomba kulinda alama ya biashara/huduma kwenye nchi nyingine na anataka tarehe aliyoombea kwenye nchi hizo/hiyo isomeke kwenye maombi aliyowasilisha hapa Tanzania atatakiwa ajaze sehemu ya "priorities" isipokuwa muda wake wa kuomba hautakiwi kuzidi miezi sita toka kuomba ulinzi kwenye hizo nchi.
- Muombaji atatakiwa kuchagua daraja la ulinzi "Nice Classification No. and description" kutegemea na aina ya bidhaa anazouza au huduma anazotoa.
- Atachagua kama atataka kulipia gharama za matangazo pamoja na za maombi ya usajili.

9. Baada yakuingiza taarifa zote atabonyeza kitufe cha endelea "proceed"

10. Mfumo utatengeneza fomu ambayo itakuwa na taarifa zote alizoingiza mteja "consolidated form" mteja atatakiwa "ku-refresh" na "kuidownload" fomu hiyo, kuprint na kuweka sahihi na endapo mmiliki ni kampuni atatakiwa kugonga muhuri wa kampuni mahala palipo sainiwa.

11. Mfumo utampeleka kwenye dirisha la kuambatanisha viambatanishi ambavyo ni; fomu "consolidated form" kwenye muundo wa "PDF", kama alama yake inamchoro atatakiwa kuambatanisha mchoro husika ukiwa kwenye muundo wa "JPEG", kama atakua anaomba "priority date" atatakiwa kuambatanisha "priority documents", kama muombaji atakuwa ni muwakilishi atatakiwa kuambatanisha fomu TM/SM 1 ya uwakilishi

12. Baada ya hapo atabonyeza kitufe cha endelea na mfumo utampeleka kwenye malipo ambapo atachagua njia gani ya malipo atakayotumia

13. Baada ya malipo maombi yatafika BRELA na mteja atapata risiti ya malipo kwenye akaunti yake ambayo anaweza kuifungua kwa kubonyeza kitufe cha "download receipt"

14. BRELA watayafanyia kazi

15. Baada ya kukamilika mteja anapokea ujumbe kwenye barua pepe na namba ya simu aliyowasilisha kwenye mfumo ujumbe utamtaarifu kama ombi lake limepitiswa ataweza pia kupata barua ya matokeo ya ombi lake sehem ya maombi (applications) kwa kufungua ombi na kufungua barua sehemu ya "printouts"

16. Kama ombi lake lina mapungufu atapewa maelekezo ya vitu vya kurekebisha, atarekebisha na kuituma tena kwajili yakufanyia kazi. Maombi yenye mapungufu yanapatikana kwenye akaunti ya mwombaji sehemu ya "my list"

## Hatua za Usajili wa Hataza kwa njia ya mtandao

1. Mtumiaji ataingia kwenye tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na kupata link ya usajili kwa njia ya mtandao
2. Mwombaji akishaingia kwenye kurasa ya usajili kwa njia ya mtandao (https://ors.brels.go.tz/ors) analazimika kufungua akaunti ili aweze kutumia huduma za BRELA zitolewazo kwa njia ya mtandao. Ili kutengeneza akaunti kwa mtanzania analazimika kuwa na namba ya utambulisho wa utaifa na kwa wasio raia wa Tanzania namba ya pasi ya kusafiria pamoja na taarifa za barua pepe, namba ya simu ya mkononi na kutengeneza nywila (password).